# AckySHINE.com

# Nini kifanyike nini kwa mtu ambaye hafikii kilele au mshindo wakati anapofanya mapenzi?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kwa mwanaume, dalili ya kufikia mshindo ni uume kusimama halafu kumwaga manii . Manii kutotoka wakati wa kujamii ana inaweza kusababishwa na mambo mengi. Kutoa manii kunatumia nguvu nyingi za mwili.

Kwa hiyo chochote kile kinachompunguzia mwanaume nguvu za mwili kama vile maradhi mbalimbali, ulevi wa pombe au dawa za kulevya, njaa au lishe duni kunasababisha mwanaume ashindwe kutoa manii . Sababu nyingine muhimu ni kutokuwa tayari kimawazo au kutokuwa na huruma katika tendo la kujamii ana. Kama ulevi ni sababu ya shida yako, jitahidi kuyaacha mambo haya. Jaribu kutulia na kuongeza muda wa kutayarishana kimapenzi mpaka mtakapoona mko tayari. Kwa mwanamke, kutofikia mshindo pia kuna sababu mbalimbali. Lakini mara nyingi i i inasababishwa na kutokuwa na subira katika maandalizi ya kujamii ana, kutokuwa tayari kimawazo au kuogopa matokeo ya kufanya mapenzi. Mwanamke akiwa tayari kimawazo kwa kujamii ana na mwanaume akijitahidi kumstarehesha vizuri, mwanamke atafikia mshindo bila shida. Pia kuwa wazi juu ya unachokipenda na usichokipenda i inasaidia sana katika kuwa na ngono ya kuridhisha kwenu wote wawili.